HOTUBA YA MHE. PROF. DAVID HOMELI MWAKYUSA (MB.) WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII WAKATI WA UZINDUZI RASMI WA MPANGO MKAKATI WA TATU WA SEKTA YA AFYA, 2009 – 2015 UKUMBI WA KARIMJEE – DAR ES SALAAM TAREHE 30 JUNI, 2009

Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Wahe. Mabalozi na Wanadiplomasia,

Makatibu Wakuu,

Wadau wa Maendeleo,

Wawakilishi wa Mashirika ya Dini, Asasi za Kujitolea na za Kijamii,

Wakurugenzi,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Ninapenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwenu kwa kuitikia wito wetu kuja kushiriki uzinduzi rasmi wa Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya Kitaifa, mpango ambao unaanza kutekelezwa 2009 hadi 2015.

Tukio hili linafanyika leo ikiwa ni takribani miaka kumi (10) ya utekelezaji wa mpango wa mabadiliko ya Sekta ya Afya

nchini ulioanza mwaka 2000. Binafsi natambua na kushukuru kuwepo kwa kila mmoja wetu katika tukio hili la kimaendeleo. **Karibuni sana.**

Mhe. Rais,

Ninayo furaha pia kukujulisha ya kwamba, mpango mmoja shirikishi, yaani "Sector Wide Approach Programme", umeweza kutekelezwa kwa mafanikio katika kipindi cha miaka kumi iliyomalizika. Mpango Mkakati wa kwanza (HSSP- I) ambao ulianza mnamo 1999 hadi 2002 ulikuwa ndio mpango wa kwanza uliotekelezwa kupitia dhana ya mpango mmoja shirikishi, yaani SWAP.

Mpango Mkakati wa pili (HSSP-II), ulitekelezwa kati ya 2003 hadi 2008. Mpango Mkakati wa tatu (HSSP-III) unaoanza 2009 – 2015 unabeba dhana ya ushirikiano katika kufikia malengo ya milenia, yaani "Partnership for delivering the MDGs". Mpango huu mpya umebainisha maeneo ya kipaumbele ambayo yatatekelezwa katika ngazi kuu tatu kama ifuatavyo:-

Ngazi ya kwanza ni Afya Wilayani ambapo katika ngazi hii kunajumuisha huduma za Afya katika ngazi ya Kaya, Kijiji na Kata.

Ngazi ya pili ni Huduma za Afya ngazi ya Mkoa na, ngazi ya tatu ni ya kitaifa. Maeneo 11 kipaumbele katika ngazi hizo tatu yaliyoainishwa katika mpango huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Huduma za Afya Wilayani
(ii) Huduma za Rufaa ikiwemo Hospitali ya Taifa
(iii) Uratibu wa kitaifa, ikiwemo kubuni sera, usimamizi na udhibiti.
(iv) Raslimali watu, ikiwemo mafunzo ya wataalam wa Afya, makisio ya raslimali watu. Lengo likiwa ni kujenga raslimali watu inayokidhi malengo ya Sekta ya Afya na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani.
(v) Raslimali fedha inayokidhi mahitaji halisi ya Sekta ya Afya, mahitaji ya jamii, ukuaji wa sekta, mabadiliko ya teknolojia, ikiwemo michango ya jamii katika kupanua na kukuza huduma za Afya nchini.
(vi) Ushirikiano baina ya sekta za umma na binafsi katika kukidhi mahitaji ya sekta ya Afya na kuhakikisha sekta binafsi inakua na kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Afya nchini.

(vii) Afya ya mama mjamzito, watoto wachanga na Afya ya mtoto ili kuhakikisha vifo vya mama wajawazito, watoto wachanga na watoto chini ya miaka mitano vinapungua kwa kiwango ambacho si tatizo tena. Mkakati huu unalenga pia kuhakikisha Afya ya uzazi inaboreshwa kwa ujumla wake.

(viii) Kukinga/kuzuia na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza ikiwemo malaria, UKIMWI, kifua kikuu na magonjwa yahusianayo na mfumo wa maisha, yaani “life styles related diseases and conditions”.

(ix) Mfumo mahsusi wa udhibiti wa majanga na ajali ikiwemo kujenga tahadhari na utayari wa kupambana na dharura za kiafya zinazoweza kujitokeza nchini.

(x) Ustawi wa Jamii na kuimarisha mfumo utakaohakikisha wananchi wasiojiweza wanalindwa na kuthaminiwa.

(xi) Mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utafiti ambao lengo kuu ni kuiwezesha Sekta ya Afya kuweza kupima mabadiliko, kubaini teknolojia mbadala na kutoa takwimu zitakazosaidia sekta ya Afya kuendeshwa kulingana na sera na malengo yake.

Mhe. Rais,

Kwa ujumla wake, mikakati hiyo niliyoibainisha ni muhimu sana ili nchi yetu iweze kufikia malengo ya milenia. Hata hivyo, mafanikio yatategemea utoaji huduma sanjari na uimarishaji wa mfumo wa huduma za Afya kwani huduma bora zinategemeana na mfumo wa huduma (Health Systems).

Mhe. Rais,

Mpango mkakati huu wa tatu utakaouzindua punde unategemewa kuifanikisha sekta ya Afya katika kuimarisha mazuri yote yaliyopatikana wakati wa mpango uliotangulia wa mabadiliko ya sekta, kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na madaraka kufikia ngazi ya chini zaidi ya ngazi ya Wilaya iliyozoeleka.

Katika kufanikisha haya yote, sekta ya Afya itashirikiana na wadau wetu 25 wa maendeleo. Miongoni mwao, wadau 11 tayari wamo katika mpango wa “Health Basket Fund” ikiwa ni ongezeko kutoka wadau watano wa awali waliokuwa katika mpango huu. Wadau wa Health Basket Fund wakiwemo wale wa “One UN” wamekuwa wakitoa mchango mkubwa kwa sekta ya Afya nchini. Kwa ujumla wadau wa

maendeleo kupitia SWAP wamekuwa wakichangia kati ya asilimia 35 na 44 ya bajeti ya sekta ya Afya nchini. Kwa mwaka ujao wa fedha, wadau kutoka nchi marafiki wa Tanzania wametoa mihadi ya Dola za Marekani milioni 61 ikilinganishwa milioni 25 zilizotolewa 2003. Kiwango hiki huenda kikaongezeka kutokana na kuwepo uwezekano wa wadau zaidi kuthibitisha kuchangia "Health Basket Fund" kwa mwaka 2009/2010. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru nchi marafiki ambao ni wadau wetu kwa michango yao katika sekta ya Afya nchini Tanzania.

Mhe. Rais,

Vile vile, napenda kukujulisha ya kwamba, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pia hupata misaada ya kitaalam kutoka wanachama 25 wa mpango mmoja shirikishi yaani SWAP kupitia umoja wao wa "TROIKA CHAIRS". Kwa misaada ya kitaalam ambayo inahitajika kutoka nje, wadau wetu wamekuwa wakilipia gharama za wataalam washauri kulingana na makubaliano na Wizara ili kuziba mapengo ya wataalam yanapojitokeza. Kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo baina ya Serikali yetu na wadau wa maendeleo yametuwezesha kufikia makubaliano ya pamoja juu ya maeneo kipaumbele ikiwemo sera ya Taifa ya Afya ya

mwaka 2007, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), Mpango wa Afya ya mama, Mtoto mchanga na watoto (MNCH) yaani “one Plan”, Mpango Mkakati wa Raslimali watu, kuimarisha kasi ya kufikia malengo ya milenia namba 4, 5 na 6 kupitia mpango wa P4P, yaani “Payment for Performance”. Mpango huu wa P4P utatekelezwa katika Halmashauri zote nchini kama inavyojieleza katika HSSP-III.

Mpango wa P4P ni miongoni mwa mikakati mingi iliyopo, unaolenga kukuza ufanisi hususani katika mazingira tete ya upungufu wa wataalam, mkakati utakaomwezesha kila mtumishi aliyepo kufanyakazi kwa bidii na ari zaidi ili kuokoa maisha ya mama wajawazito na watoto, ikiwemo watoto wachanga, na hivyo utachochea kasi ya kufikia malengo ya milenia. Kwa sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI tunaendelea kuwezesha timu za Afya za Mikoa na Halmashauri ili mpango huu wa P4P uweze kuingizwa katika mipango ya Afya ya Halmashauri kama motisha kwa watumishi wanaotoa huduma za Afya katika Halmashauri zote nchini. Ni imani yangu kuwa wadau wetu wa maendeleo kutoka nchi marafiki wataafikiana nasi na

kusaidia eneo hili muhimu linalolenga kuboresha huduma ya mama mjamzito na watoto ngazi za chini ya ngazi ya Wilaya.

Mhe. Rais,

Utekelezaji wa mpango mkakati wa tatu utahitaji vitendo katika ngazi zote kama tulivyofanya katika mipango yote iliyotangulia. Katika mpango mkakati huu, ngazi ya Kaya imebainishwa kama ngazi ya chini kabisa ya huduma na mpango wa ufuatiliaji, tathmini na utafiti umezingatiwa katika ngazi zote. Hii itawezesha kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano ili kupata takwimu sahihi, ikiwemo takwimu zitakazowezesha kupima kiwango cha mabadiliko, yaani IMPACT. Tunachohitaji sasa ni kuhakikisha tunaimarisha jitihada zetu ili kuhakikisha jamii inashiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Mhe. Rais, kwa kuzingatia umuhimu ulioipa sekta ya Afya kama moja ya sekta kipaumbele, na kujitoa kwako katika kusaidia maendeleo ya sekta ya Afya nchini, ikiwemo ongezeko la bajeti na hasa tukiwa sekta ya tatu baada ya elimu na miundombinu, tunakuhakikishia utekelezaji wa mpango mkakati wa tatu wa sekta ya Afya utakuwa wenye mafanikio. Hadi sasa, sekta ya Afya tayari imepiga hatua kubwa na mengi yameshafikiwa. Hata hivyo, tunahitajika kufanya zaidi na tunahakika mambo mengi

yanaweza kufanikishwa kutokana na sera, mikakati na jitihada za serikali, wadau wetu, watumishi wote na wananchi kwa ujumla.

Tunapenda kuchukua fursa hii ya pekee kukushukuru wewe Mhe. Rais, kwa jitihada zako na mwongozo wako katika kusaidia sekta yetu ya Afya, na kwa hakika, tunajisikia heshima na wenye furaha kwa kukubali kwako kubariki na kuzindua mpango mkakati-III wa sekta ya Afya. Hii ni ishara tosha ya kwamba kuna utashi wa kisiasa katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya sekta ya Afya.

Mhe. Rais,

Napenda sasa nichukue fursa hii kukuomba ukubali kukabidhi nakala ya HSSP-III kwa kila mdau wa maendeleo miongoni mwa wadau wetu 25, wawakilishi wa Asasi za Dini, na Asasi za kijamii zilizopo hapa, ikiwa ni ishara ya ushirikiano na kuomba ushirikiano zaidi katika kufikia malengo ya sekta ya Afya na milenia. Kwa upande mwingine Mhe. Rais, watumishi wa Afya, wake kwa waume waliopo hapa na popote nchini wako tayari kupokea maelekezo yako na kuchukua hatua sahihi kuimarisha sekta ya Afya katika ngazi zote za huduma.

Kwa wadau wetu ninayo furaha kwa kuhudhuria kwenu siku ya leo. Kuwepo kwenu wadau wa maendeleo, Wizara na Idara za Serikali, Taasisi za Umma, Asasi za Dini, Asasi za kijamii, sekta binafsi na wote mliopo, ni ishara tosha kuwa kwa pamoja tutashirikiana kutekeleza mpango huu. Nawashukuru kwa namna ya pekee kwa kuendelea kusaidia na kuchangia maendeleo ya sekta ya Afya nchini, malengo ya milenia na kupunguza umaskini nchini na hivyo kuboresha Afya ya watu wetu. Ninawashukuruni wote kwa kufika kwenu hapa.

Mhe. Rais, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi, sasa nachukua fursa hii kwa heshima na taadhima kukukaribisha rasmi uweze kuwahutubia waalikwa.

Karibu sana.